BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

<u>BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI</u>

<u>MKUTANO WA KUMI NA TANO</u>

<u>Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 26 Juni, 2024</u>
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. <u>MASWALI:</u>

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

243. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuliendeleza eneo la Zone F.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

137. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali inawashajihisha wanawake, vijana na makundi maalum kuzitumia fursa za mikopo inayopatikana katika taasisi za fedha ili kujikwamua katika shughuli mbali mbali za kibiashara. Pamoja na ushajihishaji huo, wengi wao wamekuwa wakishindwa kutimiza masharti ya dhamana ya mikopo hiyo:

(a) Je, Serikali inatambua kuwa dhamana katika taasisi hizi za fedha ni kikwazo kikubwa kwa makundi haya kupata mikopo.

(b) Je, Serikali inayasaidia vipi makundi haya kupata mikopo hii kutoka katika taasisi za fedha ili kuboresha biashara zao.

<u>**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**</u>

208. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wakulima wengi wa kilimo cha tungule Zanzibar hukumbana na tatizo la kubwaga kwa bidhaa sokoni na kushuka kwa bei ya zao hilo.

Ni lini Serikali itafikiria kuanzisha viwanda vya kusindika zao hilo kwa faida ya wakulima wetu.

286. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali iliyaingiza baadhi ya mashamba ya wananchi katika Mpango wa Hifadhi ya Misitu ya Jamii (Community Forest) na kuijumuisha katika miradi ya uvunaji wa hewa ya 'Carbon'. Pamoja na jamii kubwa kukubaliana na jambo hili zuri na Serikali kuwaahidi wananchi na wamiliki wa mashamba hayo kunufaika moja kwa moja na Mpango huo, kuna malalamiko makubwa yamejitokeza katika jamii.

(a) Je, ni upi utaratibu uliotumiwa na Serikali katika kuyaingiza mashamba haya katika hifadhi ya misitu ya jamii.

(b) Je, ni sera au sheria gani inayosimamia masuala haya ya uhifadhi wa mazingira na uhifadhi wa misitu ya jamii (Community Forest).

(c) Je, ni faida gani wamiliki watafaidika na mradi huu moja kwa moja na ni utaratibu gani utatumika kuhakikisha wananufaika.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

130. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi za kutatua changamoto ya afya katika visiwa mbali mbali vya Zanzibar kwa kutafuta boti za majini (Ambulance) ambazo lengo lake lilikuwa ni kuwasaidia wananchi wanaoishi katika visiwa hivyo, kuwafikisha kiurahisi katika vituo mbali mbali vya afya. Pamoja na juhudi hizo kumejitokea changamoto kubwa katika boti hizo.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba boti hizi hazitumiki tokea zilipopelekwa katika maeneo kama ya Bandari ya Wete na Kojani.

(b) Je, ni sababu ipi inayopelekea boti hizi kutokutumika kwa kazi iliyokusudiwa.

(c) Je, ni upi mpango wa muda mrefu wa Serikali wa kutatua tatizo la afya katika visiwa kama vile kisiwa cha Kokota.

290. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali imezibinafsisha (Outsource) baadhi ya kada kwenye hospitali zote za Wilaya Unguja na Pemba kwa lengo la kuboresha huduma za afya kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na kubadilisha tabia iliyolalamikiwa kwa muda mrefu ya baadhi ya wafanyakazi wa Wizara yako kuwa wanajeuri na wanafanya kazi zao kwa mazoea.

(a) Je, tokea Wizara yako itowe ‘Contracts’ hizo za kazi kwa makampuni mbali mbali ikiwemo LACENT, NSK pamoja na SEIFII ni kwa kiasi gani huduma za afya zimeboreka.

(b) Je, idadi ya vifo vya mama na mtoto vimepungua kwa asilimia ngapi.

(c) Je, ni madaktari bingwa wangapi wameongezeka kwa ujio wa kampuni hizo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

272. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ndani ya anga za Zanzibar, kumekuwepo FM Radio inayotangaza kupitia 97.5 MHz. Hata hivyo, Radio hii imekuwa ikirusha vipindi vichafu sana nyakati za usiku.

(a) Je, Radio hii imepewa leseni ya aina gani ya kurushia matangazo.

(b) Je, ni utaratibu upi unaotumika kuzihakiki na kuziadabisha Radio zilizopewa leseni Zanzibar zikawa zinakiuka maadili, ili kuhakikisha kwamba matangazo yao hayakinzani na makubaliano ya leseni walizopewa na ustaarabu wa Zanzibar.

(c) Je, ni vipindi gani maarufu hutangazwa na Radio hii nyakati za usiku.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

100. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na changamoto kubwa ya kupatikana maji safi na salama katika shehia ya Mtambwe Kaskazini. Shehia hii yenye idadi ya wananchi 7,473 inategemea kisima kimoja tu kilichopo katika kijiji cha Uondwe, ambacho hutoa huduma kwa vijiji 10. Hali hii inathibitisha wazi kuwa kisima hicho kimezidiwa na kusababisha shida kwa wananchi wa vijiji hivyo, pamoja na juhudi za Serikali za kuchimba kisima chengine cha ziada katika eneo la Mpakanjia kupitia mfuko wa UVIKO 19 ambacho nacho pia hakileti tija iliyokusudiwa.

(a) Je, Serikali inalitambua tatizo hili na ni upi mpango wa kulitatua tatizo hili la kupatikana maji safi na salama katika jimbo la Mtambwe.

(b) Je, ni sababu zipi zinapelekea kisima hichi kipya kilichochimbwa kupitia mfuko wa UVIKO19 kutokutumika mpaka hivi sasa.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuchimba visima katika shehia nyengine za Mtambwe Kusini na Kisiwani ili kutatua tatizo hili la maji.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

228. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Sekta ya Utalii ina jukumu kubwa katika kukuza uchumi na hatimae kufikia lengo la kupunguza umasikini kwa wananchi wetu.

Je, ni ipi mikakati ya Wizara yako katika kubuni namna ya kuvuna masoko mapya ya utalii badala ya kuendelea kuzitegemea nchi zile zile tulizozizowea.

229. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Suala la kuunda Kamati za Utalii za Wilaya kwa mantiki ya kuendeleza dhana ya utalii kwa wote liko vipi katika utekelezaji wake.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

154. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hivi karibuni, Serikali imejenga barabara nyingi za ndani nchini kwa lengo la kuwarahisishia wananchi kupita kwa urahisi, jambo ambalo limeisaidia sana jamii.

(a) Je, ni kwa hatua gani ujenzi wa barabara hizi umefikiwa.

(b) Je, viwango vya ujenzi wa barabara hizi vinakidhi vigezo vilivyotarajiwa.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

281. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Je, ni kwa kiasi gani Serikali imeweza kuongeza uzalishaji wa bidhaa hasa za viwandani kwa ajili ya mauzo ya nje ya nchi na katika soko la kikanda, kati ya mwaka 2020 na 2024.

II. **HOJA ZA KAMATI:**

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo:**

Azimio la Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**26 Juni, 2024.** **KATIBU WA BARAZA**